

# Maji ya Kunywa baada ya mafuriko

Habari juu ya wakati na jinsi ya kunywa maji kwa usalama kisha mafuriko

Swahili | Kiswahili

## OFFICIAL

Kisha mafuriko, mtoaji wako wa maji atakushauri ikiwa maji yako ya bomba ni salama ajili ya kunywa. Wanaweza kutoa:

**Ushauri wa kutokunywa maji:** Maji yako yana kemikali hatarishi (produit chimiques nuisible) na sumu na kuyanywa kunaweza kukufanya uwe mgonjwa sana.

**Ushauri kutokotesha maji:** Maji yako yanaweza kuwa na vijidudu na lazima utokoteshe maji kabla ya matumizi. Kunywa maji ambayo hayajatokotesha kunaweza kukufanya kuwa mgonjwa.

## Nini cha kufanya ikiwa huwezi kunywa maji ya bomba

Huwezi kunywa maji ya bomba ikiwa shirika lako la maji limetoa ushauri wa 'Kutokunywa maji'.

- Ni lazima
  - ✓ usinywe maji ya bomba kutoka kwa eneo liligusiwa
  - ✓ usitokoteshe, tunze maji kwa klorini au dawa ya maji (eau de javelle) kwani hayatafanya yawe salama.
- Tumia maji ya chupa kwa kunywa, kutayarisha chakula, vinywaji, na fomula ya watoto, kutengeneza barafu, kuosha meno au maji ya kunywa ya mnyama wapendwa wa nyumbani.
- Katika hali zingine, unaweza kutumia maji ya bomba kutelemusha uchafu katika vyoo (wc), kuosha mikono yako, kuoga (hakikisha usinywe maji) na kufua nguo. Acha kutumia maji na wasiliana na daktari wako ikiwa unapata kuwasha kwa ngozi au athari (réaction) nyingine yoyote.
- Mtoa huduma wako wa maji atakujulisha ni wakati gani salama wa kunywa maji yako ya bomba.

## Nini cha kufanya ikiwa huwezi kunywa maji ya bomba

Ikiwa mtowaji wako wa maji ametoa 'Ushauri wa kutokotesha maji' unahitaji kutokotesha maji yako ya bomba.

- Ili kutokotesha maji yako ya bomba ili yawe salama kunywa:
  - ✓ tokotesha maji hadi uone mapovu mengi kutoka chini ya chungu au chupa ya chai kwa muda unaoendelea.
  - ✓ polesha maji mbele ya matumizi.
  - ✓ chupa ya chai na interrupteurs automatiques moja zinafaa. Chupa za chai za joto zinazobadilika zinapaswa kuwekwa kwa kutokotesha.
  - ✓ weka maji yalio tokotesha katika chombo safi na kinacho funikiwa.
  - ✓ polesha maji mbele ya matumizi
  - ✓ fanya hange ili kuepuka vidonda vya kuunguwa.
- Maji yaliyotokotesha yanapaswa kutumika kwa ajili ya kunywa, kutayarisha chakula, vinywaji, na fomula ya watoto; kutengeneza barafu; kusafisha meno na maji ya kunywa ya mnyama wapendwa wa nyumbani.
- Maji ambayo hayajatokotesha yanaweza kutumika kunawa mikono, kuoga (hakikisha usinywe maji), kutelemusha uchafu katika vyoo (wc), kuosha vyombo na nguo na kutunza bustani au kurusha uchafu na maji ya bomba nje.
- Mtoa huduma wako wa maji atakujulisha ni wakati gani salama wa kunywa maji yako bila kutokotesha.

## Pata msaada

- Ongeya na mtoa huduma wako wa maji kwa maelezo <[www.water.vic.gov.au/water-industry-and-customers/know-your-water-corporation](http://www.water.vic.gov.au/water-industry-and-customers/know-your-water-corporation)>.
- Ikiwa una wasiwasi kuwa unaweza kuwa umetumia maji machafu au unapata dalili zinazofanana na maumivu ya tumbo, ongeya na daktari wako.

Ili kupokea chapisho hili katika muundo (format) unaofikiwa, tuma barua pepe (email)

[pph.communications@health.vic.gov.au](mailto:pph.communications@health.vic.gov.au)